OFISI YA RAIS TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA UKEREWE

Simu No: 0754561771/0621661231

Au 0754248548

Shule ya Sekondari Bukongo

S.L.P. 474,

NANSIO-UKEREWE.

Email: bukongoss@gmail.com

Kumb. Na. BSS/ADM/2018/JOIN/01

15/06/2018

NDUGU .....

.....

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO MWAKA 2018/2019

Ninayo furaha kubwa kukupongeza kwa kuchaguliwa kujiunga na **Kidato cha Tano** ..... katika **Shule ya Sekondari Bukongo** iliyopo Wilayani **Ukerewe,** Mkoa wa **Mwanza.**

Kwa kuwa wewe ni mmoja miongoni mwa wachache **waliobahatika** kuchaguliwa kuendelea na masomo ya juu ya sekondari, ni imani yangu kuwa utatumia vizuri nafasi hii uliyopewa kusoma kwa bidii kwa manufaa yako binafsi, familia yako na taifa kwa ujumla.

MAHALI SHULE ILIPO

Shule ya Sekondari Bukongo ipo kilomita mbili (2) nje kidogo ya mji mdogo wa Nansio kwa upande wa Kaskazini, ni mwendo wa kama dakika kumi kwa usafiri wa gari kutoka bandari ya Nansio au dakika tano kutoka kituo cha mabasi cha Nansio.

Usafiri kufika Mjini Nansio ni wa meli kama utatokea Mwanza mjini, na kama utatokea Bunda mkoa wa Mara, utapanda magari yanayotoka Bunda mpaka Nansio kupitia kivuko cha Kisorya.

KUFUNGUA SHULE

Shule itafunguliwa tarehe 02/07/2018 na masomo yataanza mara moja na mwisho wa kuripoti ni tarehe 16/07/2018. Iwapo hutaripoti hadi tarehe hiyo utahesabiwa kuwa umekataa nafasi uliyopewa, hivyo nafasi itahesabiwa kuwa wazi na itajazwa kwa kufuata taratibu za uchaguzi wa wanafunzi wanaochaguliwa kujiunga na shule za serikali.

MAELEKEZO MUHIMU

Siku ya kuripoti unatakiwa kuja/kukamilisha maelekezo yafuatayo;

A. ADA

Ada ni Tsh. **70,000/=** kwa mwaka au tsh **35,000/=** kwa muhula. Ada hii ilipwe kwenye akaunti iliyooneshwa kwenye jedwali lifuatalo na mwanafunzi afike na stakabadhi ya benki ya malipo husika na aikabidhi kwa mhasibu kwa ajili ya kukatiwa risiti.

MUHULA	KIASI	AKAUNTI (NMB)
I	35,000/=	Jina la akaunti: **BUKONGO SECONDARY SCHOOL** Namba ya akaunti: **31403700129**
II	35,000/=	
Jumla (mwaka mzima)	**70,000/=**	

B. MICHANGO MBALIMBALI

Michango hii iwekwe kwenye akaunti iliyooneshwa kwenye jedwali lifuatalo na mwanafunzi afike na stakabadhi ya benki ya malipo husika na aikabidhi kwa mhasibu kwa ajili ya kukatiwa risiti.

NA	MCHANGO	KIASI	AKAUNTI (NMB)
1	Wapishi (kwa mwaka)	35,000/=	Jina la akaunti: **ELIMU YA KUJITEGEMEA BUKONGO SEKONDARI** Namba ya akaunti: **31402300629**
2	Matron (kwa mwaka)	15,000/=	
3	Taaluma (kwa mwaka)	20,000/=	
4	Umeme na maji (kwa mwaka)	10,000/=	
5	Tahadhari (hairejeshwi)	10,000/=	
6	Kitambulisho	5,000/=	
7	Nembo	2,000/=	
	JUMLA	**97,000/=**	

NB: Fedha ya huduma ya kwanza ni Tsh. 20,000/=. Mwanafunzi afike na fedha hii na aikabidhi kwa mhasibu na itatumika kwa ajili ya mwanafunzi husika tu.

C. MICHANGO KWA AJILI YA SARE ZA SHULE

Michango hii iwekwe kwenye akaunti iliyooneshwa kwenye jedwali lifuatalo na mwanafunzi afike na stakabadhi ya benki ya malipo husika na aikabidhi kwa mhasibu kwa ajili ya kukatiwa risiti.

NA	SARE	IDADI	KIASI @	KIASI JUMLA	AKAUNTI (NMB)
1	Sketi za kijani	2	20,000/=	40,000/=	Jina la akaunti: **ELIMU YA KUJITEGEMEA BUKONGO SEKONDARI** Namba ya akaunti: **31402300629**
2	Sketi nyeusi	2	20,000/=	40,000/=	
3	Tai	2	2,500/=	5,000/=	
4	T-Shirt za zambarau	2	10,000/=	20,000/=	
5	T-Shirt ya kijani	1	8,000/=	8,000/=	
6	Sweta	1	15,000/=	15,000/=	
			JUMLA	**128,000/=**	

D. SARE ZA SHULE

i. Sketi mbili za rangi ya kijani iliyokolea (zitashonwa shuleni kwa gharama ya Tsh. 20,000/= kila moja kama ilivyoelekezwa kwenye michango hapo juu)
ii. Shati mbili nyeupe za mikono mirefu za tetron. Utanunua na kuja nazo shuleni na zitakaguliwa.
iii. Tai mbili za rangi ya kijani (zitashonwa shuleni kwa bei iliyotajwa kwenye michango)
iv. Viatu vyeusi vya ngozi, visiwe na visigino virefu na viwe vya kamba
v. Soksi nyeupe jozi mbili
vi. T-shirt mbili za rangi ya zambarau iliyokolea zenye ukosi kwa ajili ya kushindia (zitapatikana shuleni kwa bei ya Tshs. 10,000/= kwa kila moja kama ilivyoelekezwa kwenye michango)
vii. T-shirt moja rangi ya kijani ya ukosi wa kuzunguka iliyokolea kwa ajili ya michezo (itapatikana shuleni kwa bei ya shilingi 8,000/= tu kama ilivyoelekezwa kwenye michango)
viii. Bukta au suruali ya michezo ya kijani iliyokolea kwa ajili ya michezo. Utanunua na kuja nazo shuleni na zitakaguliwa.
ix. Raba za michezo jozi moja rangi nyeupe au nyeusi. Utanunua na kuja nazo shuleni na zitakaguliwa.
x. Sketi nyeusi kwa ajili ya shughuli zingine nje ya darasa (itashonwa shuleni kwa bei ya Tshs. 20,000/= kama iliyoelekezwa kwenye michango)
xi. Nusu kanzu nyeupe kwa wanafunzi wa kiislamu (ishone mwenyewe)
xii. Sweta moja rangi ya kijani iliyokolea (linapatikana shuleni kwa bei iliyoelekezwa kwenye michango)
xiii. Track suit moja rangi ya blue kwa ajili ya michezo/maandalio ya jioni. Utanunua na kuja nayo shuleni na itakaguliwa.

E. MAHITAJI MENGINE YA MUHIMU YA MWANAFUNZI

i. Godoro size 2.5x6 (yanapatikana pia duka la shule kwa bei ya kati ya Tsh. 35,000/= na 45,000/= kutegemeana na ujazo wake. Hivyo waweza kuja na fedha hiyo kwa ajili ya kununulia godoro)
ii. Sanduku moja la chuma kwa ajili ya kuhifadhia vifaa vya mwanafunzi (tranka) pamoja na kufuli lake
iii. Mashuka matatu rangi ya light blue
iv. Ndoo mbili lita 10 kwa matumizi binafsi na matumizi ya shule
v. Galoni (lita 5) ya kuhifadhia maji ya kunywa
vi. Chandarua cha rangi nyeupe
vii. Sabuni za kuogea na kufulia za kutosha, mswaki, ndala, dawa ya meno na mafuta ya kupaka pamoja na mahitaji yake muhimu
viii. Mto mmoja na foronya yake yenye rangi ya light blue
ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe)
x. Taulo
xi. Tochi au taa ya sola kwa ajili ya mwanga siku umeme ukikatika.

F. VIFAA VYA TAALUMA

Mzazi anashauriwa kumnunulia mwanae vifaa vifuatavyo ili viweze kumsaidia mwanafunzi katika kujifunza.

i. Vitabu vya kiada na ziada kwa masomo yake
ii. Madaftari makubwa (counter books) nane (8) zenye kurasa nyingi za kutosha
iii. Kalamu za wino (blue au nyeusi), penseli, zana za hisabati (mathematical sets) kwa wanafunzi wa mchepuo wa sayansi
iv. Scientific calculator kwa wanafunzi wa mchepuo wa sayansi
v. File cover moja
vi. Karatasi bunda moja (duplicating paper) kwa mwaka lenye karatasi 500 (A_4) kwa ajili ya matumizi ya ofisi kama vile mitihani, ripoti n.k. Utakabidhi unaporipoti (hatupokei fedha).

G. VIFAA VYA USAFI

i. Kidato cha tano HKL watakuja na jembe pamoja na reki vikiwa na mipini yake pamoja na fyekeo moja.
ii. Kidato cha tano CBG watakuja na mifagio laini (soft blooms), brashi ngumu, mopper pamoja na mifagio ya chelewa.

MUHIMU:

Siku ya kuripoti unatakiwa kuja na kukabidhi vitu vifuatavyo;

i. Cheti halisi cha kumaliza kidato cha nne (original form four leaving certificate) pamoja na kivuli chake
ii. Cheti halisi cha kuzaliwa (original birth certificate) kiambatane na kivuli chake
iii. Original form four results slip na kivuli chake.
iv. Fomu ya maelezo binafsi iliyojazwa vizuri na kwa usahihi (imeambatishwa FOMU Na. B)
v. Fomu ya uthibitisho wa afya ya mwanafunzi (Medical examination form) iliyojazwa kikamilifu na kugongwa muhuri na mganga mkuu wa Wilaya/Mkoa au hospitali ya rufaa (imeambatishwa FOMU Na. C)
vi. Picha mbili za rangi (passport sized) zenye pazia la bluu (blue background) zilizopigwa hivi karibuni. Ziandikwe majina kamili ya mwanafunzi nyuma yake.

KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI BUKONGO

MOTTO: *"ELIMU KWA MAENDELEO"*

.....

Emmanuel B. Malubalo

MKUU WA SHULE.

HEADMASTER
BUKONGO SECONDARY SCHOOL
Box 474
NANSIO

FOMU Na -A-

SHERIA ZA SHULE

1. Mwanafunzi anatakiwa kuwepo eneo la shule wakati wote isipokuwa anapopata ruhusa maalumu kutoka kwa mwalimu wa zamu, matron, mwalimu wa darasa, makamu mkuu wa shule, au mkuu wa shule.
2. Mwanafunzi anapaswa kuvaa sare rasmi ya shule muda wote wa darasani, isipokuwa muda wa kazi za mikono au michezo ambapo atavaa nguo rasmi za kazi/michezo
3. Lugha chafu, matusi, ugomvi, fitina na kupigana kwa mwanafunzi **HAVIRUHUSIWI**
4. Ni lazima kwa mwanafunzi kuwahi popote anapotakiwa na kwa kwa wakati uliowekwa
5. Ni lazima kwa mwanafunzi kuheshimu kazi ya darasani na nje ya darasa na kuifanya kwa kwa ufanisi. Ni lazima kufanya mazoezi/majaribio yote yanayotolewa darasani awapo shuleni.
6. Unywaji wa vileo, na uvutaji wa sigara, bangi na madawa yoyote ya kulevya ni MWIKO kwa mwanafunzi.
7. Wizi wa aina yoyote hauruhusiwi kwa mwanafunzi
8. Ni kosa kwa mwanafunzi kupoteza au kuharibu mali binafsi au mali ya umma
9. Ni marufuku kushiriki au kuendekeza imani za kishirikina shuleni
10. Ni marufuku kwa mwanafunzi kufanya unyanyapaa au uonevu wa aina yoyote kwa mwanafunzi mwenzake.
11. Mwanafunzi anapaswa kuwa na heshima na mtiifu wakati wote na kwa kila mtu. Ni marufuku kukaidi au kubishia viongozi halali waliopo shuleni.
12. Mwanafunzi haruhusiwi kuolewa. Aidha ni marufuku kwa mwanafunzi kuwa na mahusiano ya kimapenzi katika kipindi chote cha uanafunzi wake. Ikibainika atafukuzwa shule mara moja.
13. **Mwanafunzi haruhusiwi kuwa na simu ya mkononi kwa kipindi chote cha uanafunzi wake. Ikibainika kuwa anamiliki simu, atafukuzwa shule mara moja.**
14. Ni marufuku kwa mwanafunzi kwenda nyumba za walimu au wafanyakazi wasio walimu bila ruhusa au kibali kutoka kwa mwalimu wa malezi/uongozi wa shule
15. Ni marufuku kwa mwanafunzi kuvaa mapambo ya aina yoyote, kufuga kucha, kupaka kucha rangi, kuvaa kofia, vitambaa au mavazi yasiyo ya heshima muda wote wa uanafunzi wake.
16. Wageni wa wanafunzi wanaruhusiwa kuonana na wanafunzi baada ya kujitambulisha na kupokelewa na makamu wa mkuu wa shule. Tunashauri wanafunzi kutembelewa siku za Jumamosi, Jumapili na siku za sikukuu ili kuondoa usumbufu siku za masomo.

MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

Yafuatayo ni makosa ambayo mwanafunzi akifanya atalazimika kufukuzwa shule;

1. Wizi wa mali yoyote ya shule au ya mtu yeyote
2. Kujihusisha na uasherati
3. Kuwa na simu ya mkononi shuleni
4. Ulevi wa aina yoyote ile
5. Uvutaji bangi na matumizi ya madawa ya kulevya
6. Kufanya makosa yoyote ya jinai kama vile kupigana, kupiga au kupiganisha
7. Kuharibu kwa makusudi mali ya shule au mali ya mtu yeyote
8. Kutoheshimu bendera ya taifa, wimbo wa taifa, nembo ya taifa au picha za viongozi wa kitaifa
9. Kuolewa
10. Kupata mimba ndani au nje ya shule
11. Kutoa mimba
12. Kukataa adhabu kwa makusudi
13. Kugoma, kuchochea na kuongoza migomo au mikusanyiko yenye kuashiria uvunjifu wa amani ndani na nje ya mipaka ya shule

FOMU Na -B-

TAARIFA MUHIMU ZA MWANAFUNZI

Shule inapenda kupata taarifa muhimu za kila mwanafunzi kwa ajili ya kufanya mawasiliano kipindi chote awapo shuleni au nje ya shule. Fomu hii ijazwe kwa usahihi na ukamilifu.

A. TAARIFA ZA MWANAFUNZI

i. Jina la mwanafunzi ..... Jinsi ..... Kidato..... mchepuo..... mwaka.....
ii. Tarehe ya kuzaliwa ..... (siku/mwezi/mwaka)
iii. Anuani ya nyumbani (anayotumia) .....
iv. Mtaa/kijiji anachotoka ..... kata..... tarafa ..... Wilaya ..... mkoa .....
v. Shule ya sekondari aliyotoka mwanafunzi ..... anuani ya shule hiyo .....
vi. Namba ya mtihani ya kidato cha nne .....
vii. Kabila .....
viii. Dini ..... (mkristo, muislamu, n.k)
ix. Dhehebu .....
x. Uraia ..... (Mtanzania, n.k)

B. TAARIFA ZA MZAZI/MLEZI

(Bandika picha ndogo 'passport sized' ya mzazi/mlezi pembeni mwa maelezo haya)

i. Jina la mzazi/mlezi .....
ii. Anuani yake .....
iii. Namba ya simu .....
iv. Kazi anayofanya .....
v. Wilaya/mji anakofanyia kazi .....
vi. Anuani ya kazini .....
vii. Namba ya simu ya kazini .....

C. NDUGU WA KARIBU AMBAO UNGEPENDA WAPATE TAARIFA ZAKO ZAIDI YA WAZAZI/WALEZI WA KARIBU

i. Jina ..... anuani .....
Namba ya simu ..... kazi anayofanya .....
Uhusiano wako na yeye .....

ii. Jina ..... anuani .....
Namba ya simu ..... kazi anayofanya .....
Uhusiano wako na yeye .....

iii. Jina ..... anuani .....

Namba ya simu ..... kazi anayofanya .....
Uhusiano wako na yeye .....

KUMBUKA: ***Iwapo mmoja wapo wa mzazi/mlezi au ndugu wa karibu amehama au amefariki, mwanafunzi atalazimika kutoa taarifa na kubadili jina na kuandika mtu mwingine ambaye atawajibika kwake.***

D. TAMKO NA AHADI YA MWANAFUNZI

Mimi (jina) ..... **NAKUBALI** nafasi niliyopewa katika Shule ya sekondari Bukongo. Naahidi kuwa nitazitii taratibu, kanuni na sheria zote za shule. Nitafuata masharti yote yanayotolewa na Mkuu wa shule, wafanyakazi wote na viongozi wote wa shule. Ninaahidi pia nitashirikiana na wanafunzi wenzangu katika shughuli za masomo, kazi za nje na katika michezo kwa muda wote nitakaokaa Bukongo sekondari. Nakiri kuwa kwa akili zangu timamu, taarifa zote nilizotoa hapo juu ni sahihi na zinanihusu.

Jina ..... sahihi ..... Tarehe .....

FOMU Na. –C-

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

MINISTRY OF EDUCATION, SCIENCE, TECHNOLOGY AND VOCATIONAL TRAINING

BUKONGO SECONDARY SCHOOL

MEDICAL EXAMINATION FORM

(To be completed by a Medical Officer)

Student's name……..

Age …… Sex ……

Blood count (white and red) ……..

Urine ……

VD Test ……...

TB Test ……

Chest ……

Eye ……

Spleen ……..

Additional information: for instance physical defects or chronic family diseases, pregnancy etc
……
……
……
……
……..

I certify that I have examined the above mentioned student and I recommend that she is fit/unfit to pursue further education.

Name ……

Signature ……

Designation ……..

Official stamp ……

Date ……